JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

**Simu:** 026-2322129
**Nukushi**: 026-2322128
**Tovuti**: www.michezo.go.tz
**Baruapepe:** km@michezo.go.tz

Mji wa Serikali - Mtumba
Mtaa wa Michezo,
S. L. P. 25,
40481 DODOMA.

Tarehe: 18 Septemba, 2026 - Dodoma

## TAARIFA KWA UMMA

# KUHUSU JEZI ZA TIMU ZA TAIFA

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo inapenda kutoa ufafanuzi kuwa, Mhe. Paul Christian Makonda (Mb), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, hatambui matangazo ya Jezi za Timu za Taifa kutokana na mchakato wa kuzibadilisha jezi hizo kutoishirikisha Wizara licha ya maelekezo aliyoyatoa mwezi Februari 2026.

Katika maelekezo hayo, Mhe. Makonda alielekeza kwamba, kwa kuwa Serikali inawekeza fedha nyingi katika maandalizi ya Timu za Taifa zinazoshiriki mashindano ya Kimataifa na kwa kuwa Tanzania itakuwa mwenyeji wa mashindano makubwa ya Kombe la Mataifa ya Afrika, mwaka 2027 (AFCON 2027) kuna haja ya kuboresha jezi za timu za taifa ili ziakisi manufaa mapana kwa nchi.

Pamoja na kutoutambua utambulisho wa jezi za timu ya taifa, Waziri Makonda ataunda Kamati ya kuchunguza mkataba wa mzabuni wa jezi hizo, ili kubaini manufaa ya mkataba huo kwa timu za taifa ambazo zimekuwa zikigharamiwa na Serikali kwa fedha nyingi licha ya uwepo wa fursa ya mauzo ya jezi yanayopaswa kuchangia katika uendeshaji wa timu za taifa.

Digitally Signed By Zaituni Mkwama
Fri Sep 18 11:13:58 EAT 2026

Zaituni Mkwama
**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**